Español Français

Mr. James D. Wolfensohn

Raisi

The World Bank Group [Mshikano wa Benki ya Dunia]

James D. Wolfensohn, raisi wa tisa wa Mshikano wa Benki ya Dunia tangu 1946, alistawi kazi yake kama mwanabenki wa kimataifa wa uwekezaji kwa kujihusisha na mambo ya maendeleo na mazingira ya ulimwengu. September 27, 1999, Bw. Wolfensohn alichaguliwa tena bila kupingwa na Bodi za Wakurugenzi Watendaji wa Benki kwa muhula wa pili wa miaka mitano kama raisi kwanzia mwanzo wa Juni 1, 2000. Atakuwa raisi wa tatu katika historia ya Benki kuketi kwa muhula wa pili.

Tangu awe raisi Juni 1, 1995, amesafiri katika nchi zaidi ya 100 ili aweze kupata ujuzi matatizo yanayoikabili Benki ya Dunia, na nchi wanachama wake 184. Katika safari zake Bw. Wolfensohn amezuru miradi ya maendeleo inayo fadhiliwa na Benki ya Dunia na pia amekutana na wateja wa kiserikali wa Benki, pamoja na wakilishi wa biashara, leba, vituo vya habari, non-governmental organizations (NGO) [mashirika yasiyokuwa ya kiserikali], makundi ya kidini na ya kina mama, wanafunzi na walimu. Katika shughuli hizi zake amefanya bidii ya kubuni ushirika upya wa muhimu kati ya Benki na serikali inazozishughulikia sekta ya kibinafsi, watumishi wa umma, benki za maendeleo ya nchi na Umoja wa Mataifa.

Katika mwaka 1996, pamoja na International Monetary Fund (IMF) [Shirika la Kimataifa la Fedha], Bw. Wolfensohn alianzisha Heavily Indebted Poor Countries (HIPC) Initiative [Hatua ya Nchi Zenye Madeni Makubwa] kama mradi wa kwanza kamili wa upunguzaji wa madeni kushughulikia mahitaji ya masikini ulimwenguni na kwa sana, nchi zenye madeni makubwa. Miaka miwili baadaye, aliongoza ukaguzi wa kilimwengu ya HIPC Initiative, iliyoshirikisha makundi ya kanisa, NGO, na wasiriki kutoka kwenye nchi watoa mikopo na zile za HIPC, ili kukagua maendeleo yake na kutafuta namna za kuboresha upana na hadhi ya mradi. Ukaguzi huu, pamoja na maoni kutoka kwa nchi wafadhili, ulisababisha kupitishwa kwa idhini rasmi September 1999 katika Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na ya IMF kuongeza maradufu kiwango cha msaada, kuruhusu nchi zaidi ili ziweze kupata misaada, na kuharakisha shughuli hii.

Januari mwaka 1999, Bw. Wolfensohn alianzisha Comprehensive Development Framework (CDF) [Mfumo wa Jumuiya wa Maendeleo] kwa kutumia maarifa ya maendeleo nakutekeleza mambo muhimu yaliyoelezwa katika hotuba zake za Mikutano ya Miaka ya 1997 na 1998. Pamoja na washiriki wengine wa Benki, CDF kwa wakati huu inafanyiwa majaribio katika nchi 13.

CDF inatilia mkazo mpango ulio kamili tena wa mda mrefu; nchi inayo ongoza imiliki na iongoze ajenda ya maendeleo; ushiriki wa nguvu zaidi kati ya serikali, wafadhili, utumshi wa umma na sekta ya kibinafsi katika kutekeleza mpango wa nchi; na mwelekeo ulio na uaminifu wa kupata matokeo ya maendeleo. Mwelekeo wa CDF

inapeana msingi wa pamoja wa ketekeleza shirikiano mpya kati ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea ndiyo kupatikane mabadiliko mema yenye kudumu katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini, ambako kutasaidia nchi zifikie Malengo ya Millennimu ya Maendeleo.

Bw. Wolfensohn ameweka kupunguza kwa kudumu kwa umasikini kuwa katika kiini cha nia ya Benki na ameelekeza shughuli za shirika hili katika kusaidia juhudi za jumuiya ya kimataifa kufikia Malengo ya Millennium ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa. Malengo yanataka kuwe na upunguzaji wa umasikini kwa nusu ya kiasi chake na kuimarishwa kwa kudumu kwa afya na elimu katika nchi zinazoendelea kufikia mwaka 2015.

Kufikia malengo hayo, Bw. Wolfensohn ameziomba nchi tajiri wafadhili ziongeze msaada wa kigeni wa maendeleo, waimarishe mipango ya misaada na wapunguze vikwazo vya kibiashara. Ameziomba nchi zinazoenedelea ziandae mageuzi muhimu ya sera ili kusaidia kukua (kwa uchumi) ndio ziweze kushughulikia kupunguza umasikini, na pia kuweza kuchangia kuimarisha huduma za afya na elimu kwa wananchi wote.

Bw. Wolfensohn ameongoza juhudi nyengine kadhaa katika Benki ya Dunia, ikiwepo Development Gateway [Mlango wa Maendeleo], Global Development Learning Network [Mtandao wa Elimu ya Maendeleo ya Ulimwengu], Dialogue on Faiths and Development [Mashauri kuhusu Imani na Maendeleo], Culture and Peace [Utamaduni na Amani].

Kabla ya kujiunga na Benki, Bw. Wolfensohn alikuwa mwanabenki wa uwekezaji wa kimataifa. Katika adaraka yake ya mwishoni yalikuwa Raisi na Mtendaji Mkuu wa James D. Wolfensohn Inc, kampuni yake mwenyewe ya uwekezaji iliyobuniwa mwaka 1981 kupeana wasia kwa mashirika makubwa ya kiamerika na ya kimataifa. Alisimamisha shughuli zake katika kampuni hiyo alipojiunga na Benki ya Dunia.

Kabla kuanzisha kampuni yake mwenyewe Bw. Wolfensohn aliwahi kuwa na madaraka aina mbalimbali ya ngazi ya juu katika mambo ya fedha. Alikuwa Mshiriki wa Uendeshaji wa Salomon Brothers huko New York na akawa mkuu wa idara yake ya shughuliza uwekezaji wa kibenki. Alikuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Uendeshaji na Meneja Msimamizi wa Schroeder’s Ltd huko London, Raisi wa J. Henry Schroeder’s Banking Corporation katika New York, na Meneja Msimamizi wa Darling & Co ya Australia.

Wakati wote katika kazi zake, Bw. Wolfensohn amejishirikisha sana na mambo aina mbalimbali ya kazi za kujitolea na sanaa haswa tamthilia. Katika mwaka wa 1970, Bw. Wolfensohn alishughulika na Carnegie Hall ya New York, mwanzoni kama mwanachama wa Bodi, na baadaye kuanzia mwaka wa 1980 hadi 1991, alikuwa Mwenyekiti wa Bodi. Huu ulikuwa wakati alipoongoza juhudi za urekebishaji na kulinda jingo hili la New York. Wakati huu yeye ni Mwenyekiti Masuhuri wa Carnegie Hall. Katika mwaka wa 1990, Bw. Wolfensohn alikuwa mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa John F. Kennedy Center for the Performing Arts in Washington, DC. Na Januari 1, 1996, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti Masuhuri.

Bw. Wolfensohn amekuwa Raisi wa International Federation of Multiple Sclerosis Societies [Muungano wa Kimataifa wa Vyama vya Multiple Sclerosis], Mwenyekiti wa Business Council for Sustainable Development [Taasisi ya Biashara kwa Maendeleo Stawi], na akafanya kazi oia kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na pia kama

Mwenyekiti wa Rockefeller Foundation na wa Population Council, na pia kama mwanachama wa Bodi la Rockefeller University [Chuo Kikuu cha Rockefeller].

Kwa wakati huu, pamoja na kuwa Raisi wa Mshikano wa Benki ya Dunia, yeye ni Mwenyekiti Bodi la Institute for Advanced Study [Taasisi ya Mafunzo Ya Ziada] katika chuo cha Princeton. Bw. Wolfensohn pia ni Mdhamini Rasmi wa Brookings Institution na mwanachama wa Council on Foreign Relations [Idara ya Uhusiano wa Kigeni] na pia wa Century Association katika New York.

Mzaliwa wa Australia, mwezi Desemba mwaka wa 1933, Bw. Wolfensohn amukuwa mwananchi wa Marekani. Ana shahada ya BA na ya LLB kutoka Chuo Kikuu cha Sydney na pia ana MBA kutoka Harvard Graduate School of Business [Cho Kikuu cha Biashara cha Harvard].

Kabla ya kusomea Harvard, alikuwa wakili katika kampuni ya sheria ya Australia Allen Allen & Hemsley. Bw. Wolfensohn alifanya kazi kama ofisa katika Royal Australian Air Force [Jeshi la Anga La Australia], na alikuwa mwanachama wa timu ya Australia ya fencing ya Olimpiki ya 1956. Bw. Wolfensohn ni Mwanachama wa American Academy of Arts and Sciences na pia ni Mwanachama wa American Philosophical Society [Chama cha Kiamerika cha Filosofia]. Amepokea tuzo nyingi kwa nazi yake, ikiwemo zawadi ya kwanza ya David Rockefeller Prize of the Museum of Modern Art huko New York kwa kazi yake katika utamaduni na sanaa.

Mei mwaka wa 1995 alipewa tuzo ya Honorary Knighthood na Malikia Elizabeth wa Pili kwa mchango wake katika sanaa. Serikali za Australia, Ufaransa, Ujerumani, Morocco, na Norway pia nazo zimemupa tuzo Bw. Wolfensohn.

Yeye na mke wake, Elaine, mtaalamu wa elimu aliyefuzu kutoka Wellesley, BA, na Columbia University, MA na Med, wana watoto watatu- Sara, Naomi, na Adam.